



(Workers' Compensation Factsheet - Swahili – 8-30-2007)

Kazi salama – Haki za wafanyakazi

Huduma Za Tibabu na Ulemavu kwa wafanyakazi waliyo umia

Ukiwa uliumia au mugonjwa ukiwa kazini, Fidia ya wafanyakazi inalipa bili yako. Pia inalipa 60 % ya mushahara ambao ungelipwa ikiwa hukwenda kazini kwa muda wa siku tatu. Fidia ya wafanyakazi ni *insurance* ambayo Mawajili wote lazima waonyeshe

Fidia ya wafanyakazi inawashugulikiya wafanyakazi wote.

Hajjali ni nani amesababisha ajali. Wafanyakazi wote wanaweza kupata Fidia, pamoja na wanaofanya kazi nusu-siku, wanaofanya kazi kwa muda mufupi, na wafanyakazi wasiyokuwa wana inchi. Wale ambao hawana ruhusa ya kufanya kazi wana weza kupewa karibu aina zote za Fidia ya Wafanyakazi

Kuripoti matukio ya ajali

Ukiwa umeumiya kazini, muambiye muajili wako. Jaza ripoti ya ajali (Form-8a WCA) haraka saana. Unaweza kupata hiyo form kutoka kwa muajili wako. Hakikisha umeweke kopi yako. Unawo muda wa myaka miwili ku ripoti ajali za kazini na ugonjwa, lakini ni vyema kuripoti haraka iwezekanavyo.

Kumuona Daktari

Una haki ya kuchagua Daktari wako ukiwa umeumia ukiwa kazini. Na pia unahaki ya kupata mawaiza ya mutu mwengine. Mara nyingi unaweza kuchaguwa daktari yoyote. Kwa wale wanao Fidia ya Wafanyakazi pamoja na utunzaji wa unaopangwa (workers' compensation with managed care), wanatakiwa kuchagua kutoka kwa orodha ya ma daktari. Hakikisha umemwambiya daktari, hospitali na wafanya kazi wa afya wengine kama kuumia kwako kumesababishwa na kazi. Bili zinatakiwa zitumwe kwa muajili, siyo kwako wewe.

Ikiwa ajali yako ao ugonjwa umesababishwa na kazi unayo fanya, hakikisha ripoti ya daktari inaelezea hivyo. Hakikisha inatowa maelezo yanayo faa kuhusu hajali yako. Ripoti hiyo iseme pia kama unatakiwa rudi kazini na kama kuna kazi ambazo haustahili kufanya kutoka na ajali yako. Mpe haya maelezo muajili wako. Muajili wako anatakiwa kuyafatiliya kwa makini maelezo ya daktari.

Kurudi kazini

Hakikisha unachukua kibarua (Form:75WA) kutoka kwa daktari wako kinayo kupa ruhusa ya kurudi kazini, na kama kuna kazi ambazo haruhusiwe kufanya kutokana na kuumiwa kwako. Umupe kopi muajili wako na uweke kopi yako mwenyewe. Muajili wako anatakiwa kufuata kwa makini maelezo ya daktari.

Kama ombi lako limekataliwa (halikukubaliwa)

Kama Wanaotoa huduma za Fidia ya Wafanyakazi wamekataa ombi lako, usikate tamaa. Baadhi Kampuni za *insurance* wanakataa ombi nyingine ili ukate tamaaa. Unaweza kukata rufani kwenye wizara ya kazi ya New Hampshire. Karibu nusu ya wafanya kazi walioumia kazini wanaokata rufani kwa wizara hiyo hushinda. Una muda wa kupita myezi kumi na nane kukata rufani.

Kupata musaada wa kisheria

Ukihitaji wakili, tafuta aliye mujuzi wa Fidia ya wafanyakazi. Hutatakiwe kulipa kabla ya huduma ya wakili. Wakili atalipwa 20 % ya malipo utakayo pewa kutokana na ajali yako kama akishinda. Akishindwa rufani yako, hautalipa wakili chochote.

Musaada toka Wizara ya Kazi ya New Hampshire

Kwa maelezo zaidi, wapiggiye simu Wizara ya Kazi ya New Hampshire nambari: 271-3176. Uliziye ukurugenzi unaoshugulika na Ombi la Fidia ya Wafanyakazi. Au nenda kwa mutandaa wa internet *www. Labor.state.NH.us*